

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI**



**WARAKA NA. 2 WA MWAKA 2025 KUHUSU MATUMIZI YA**  
**WAVU WA UVUVI (UVUNAJI) WA DAGAA KWENYE ZIWA TANGANYIKA**

*(Chini ya Kifungu cha 4(3) cha Sheria ya Uvuvi, Sura 279)*

2. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), chini ya matakwa Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Sura 1 (Toleo la 2005) na matakwa ya Sheria ya Uvuvi, Sura 279 (kama ilivyorekebishwa), ina jukumu adhimu, la kusimamia, kulinda, kuhifadhi, na kuendeleza mali asili (ikiwa ni pamoja na rasilimali za uvuvi) inayomilikiwa kwa pamoja na wananchi. Vile vile, Mkurugenzi wa Uvuvi amepewa mamlaka ya kisheria kutoa Nyaraka na Miongozo mbalimbali kwa kadri ya uhitaji ili kuhakikisha kwamba, rasilimali za uvuvi zinaendelezwa, kusimamiwa, kuhifadhiwa na kutumiwa kwa njia endelevu kwa ajili ya ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi.
3. Hali ilivyo kwa sasa imeonekana kwamba kuna changamoto zinazotokana na uvuvi wa dagaa kwa kutumia wavu wa mtando (*ring net*) na kipe (*lift nets*) usiokuwa na ukomo wa urefu na kina. Hali hii inasababisha wavuvi kuvua kwa wingi dagaa wachanga na aina nyingine ya samaki wasiokusudiwa. Inafafanuliwa kwamba endapo hakutakuwa na hatua mahususi na za makusudi, jambo hili litasababisha uharibifu wa mazalia ya samaki, makulia, na kuharibu uhifadhi wa mazingira, na hivyo kuhatarisha uendelevu wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Tanganyika.
4. Hivyo basi, Waraka huu unaainisha matumizi sahihi ya wavu wa dagaa aina ya mtando (*ring net*) na kipe (*lift net*) katika Ziwa Tanganyika, ikiwa ni hatua za usimamizi wa hifadhi ya rasilimali za uvuvi na uvuvi endelevu nchini, kama ilivyofafanuliwa hapa chini:-
  - (a) Wavu wa dagaa aina ya mtando (*ring-net*) utakuwa na urefu usiozidi mita mia moja na ishirini ( $\leq 120m$ ) na kina kisichozidi mita sitini ( $\leq 60m$ );
  - (b) Umbali kati ya boya na boya usiwe chini ya sentimita ishirini ( $\geq 20cm$ );
  - (c) Aidha, wavu wa dagaa aina ya kipe (*lift net*) utakuwa na urefu usiozidi mita hamsini ( $\leq 50m$ ) na kuwa na kina cha mita ishirini na tano ( $= 25m$ );
  - (d) Vile vile, uvuvi wa kutumia wavu wa kipe (*lift net*) au mtando (*ring-net*) ufanyike katika umbali usiopungua mita elfu moja ( $\geq 1,000m$ ), yaani, sawa na umbali usiopungua kilomita moja ( $\geq 1km$ ) kutoka kwenye ufukwe wa Ziwa Tanganyika;
  - (e) Kwamba, kwa vyovyote vile, ukubwa wa tundu la wavu usipungue milimita nane ( $\geq 8mm$ ) kwa nyavu ya mtando (*ring net*) na kipe (*lift net*); na
  - (f) Kwamba uvuvi wa aina hii hautoruhusiwa kufanyika muda wa mchana na hauruhusiwi kufanyika wakati wa mbalamwezi kwa mujibu wa Kanuni ya 66(1) ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 ikisomwa pamoja na marekebisho ya Kanuni ya 16(d)(mm) na (nn) ya Kanuni za Uvuvi iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali (GN) Na. 492 ya 03/07/2020.
5. Inafafanuliwa ya kwamba Waraka huu utanza kutumika tarehe **7 Aprili 2025** kwenye maeneo yote ya Ziwa Tanganyika na kwamba ukiukwaji wa Waraka huu ni kosa kisheria.

Prof. Mohammed A. Sheikh  
**MKURUGENZI WA UVUVI**